www.vpo.go.tz

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

MUUNGANO NA MAZINGIRA TOLEO NO..32 FEBRUARI 2020

# Rais Shein, Zungu kudumisha Muungano

Uk.2






Soma
Uk. 3



# Rais Shein, Waziri Zungu kudumisha Muungano

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ameahidi kumpa ushirikiano Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu ili aweze kutekeleza vyema majukumu husussan ya Muungano.

Dkt. Shein alisema hayo Ikulu ya Zanzibar alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri Zungu ambaye aliteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ili kushika wadhifa huo.

Alisema miongoni mwa majukumu yake makubwa aliyonayo ni pamoja na kuhakikisha Muungano unadumishwa na hivyo kuhakikisha jitihada za waasisi wake, Hayati Mzee Abeid Amani Karume na Hayati Julius Kambarage Nyerere zinaendelezwa na zinadumishwa.

Rais Dkt. Shein aliongeza kuwa Muungano umeleta mafanikio makubwa hasa ikizingatiwa kwamba walioungana ni wananchi wa pande mbili ambao wana udugu wa asili na historia ya muda mrefu.

Pamoja na hayo pia alieleza matarajio yake makubwa aliyonayo kutokana na utendaji kazi na uzoefu alionao Waziri huyo ukiwemo uzoefu wa utumishi Serikalini pamoja na ule wa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisisitiza undugu wa wananchi wa pande mbili za Muungano ni vyema ukaimarishwa na kudumishwa sambamba na kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya pande hizo mbili za Muungano.

Kwa upande wake Waziri Zungu ambaye alikuwa ameambatana na Mkurugenzi wa Muungano Ofisi hiyo Balozi Mbarouk Nassor, alimshukuru Rais Dkt. Magufuli pamoja na Rais Dkt. Shein kwa uteuzi huo huku akiahidi kufanya kazi kwa ufanisi.

Waziri Zungu aliahidi kuhakikisha changamoto ndogo ndogo zinazowasumbua wananchi hususan wafanyabiashara zinafanyiwa kazi.

# MWONGOZO WA TUZO YA RAIS YA KUHIFADHI MAZINGIRA

## MADHUMUNI YA TUZO

Madhumuni makuu ya Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ni kuongeza kiwango cha ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi mazingira ili kulinusuru taifa letu na majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira. Kupitia Tuzo hii, wananchi watahamasika kushiriki katika shughuli za kuhifadhi mazingira katika maeneo yao kwa lengo la kuboresha hali ya mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira watapatikana kutokana na juhudi za kuhifadhi mazingira katika maeneo yafuatayo:

- Hifadhi ya vyanzo vya maji na matumizi ya maji;
- Upandaji miti;
- Uzalishaji endelevu viwandani;
- Matumizi ya nishati mbadala;
- Uchimbaji madini endelevu;
- Kilimo endelevu na usimamizi wa taka; na
- Ufugaji endelevu na Afya na Usafi wa Mazingira.

## VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KUTATHMINI

Vigezo vitakavyotumika kuwapata washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ni;-

**Matumizi ya teknolojia sahihi na endelevu** katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, uzalishaji endelevu viwandani, matumizi ya nishati mbadala, uchimbaji wa madini, kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira.

**Ubunifu katika matumizi ya mbinu za asili za kuhifadhi mazingira** katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, Uzalishaji endelevu viwandani, Matumizi ya nishati mbadala, Uchimbaji wa madini, Kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira

**Utafiti wenye matokeo chanya** katika masuala ya kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, Uzalishaji endelevu viwandani, Matumizi ya nishati mbadala Uchimbaji wa madini, Kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira

**Ujasiriamali/mbinu za uzalishaji rasilimali** katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, uzalishaji endelevu viwandani, Matumizi ya nishati mbadala, Uchimbaji wa madini, Kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati na ufugaji utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira

**Elimu ya mazingira/utekelezaji wa Sheria za Mazingira**;- Utoaji wa elimu ya Mazingira, uelewa wa sheria ya mazingira zinazohusu shughuli za mshiriki, utekelezaji wa sheria ya mazingira na uwepo wa sheria ndogo za mazingira na utekelezaji wake katika kuhifadhi vyanzo vya maji, matumizi ya maji, kupanda miti na kuitunza, matumizi ya nishati, uchimbaji wa madini, kilimo, usimamizi wa taka, uzalishaji na matumizi ya nishati, ufugaji, utunzaji wa afya na usafi wa Mazingira.

**Uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake** katika shughuli za uzalishaji viwandani na migodini.

INAENDELEA UK. 4

Washindi waliopendekezwa kufikia ngazi ya Taifa watashindanishwa ili kupata mshindi wa kwanza hadi wa tano. Mshindi wa kwanza atachaguliwa kutokana na ubunifu wake wa ziada katika kuhifadhi mazingira kwa ujumla.

Wananchi wote katika ngazi mbalimbali watahamasishwa ili kushiriki kwenye mashindano haya. Aidha, Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi na vyombo vya habari vitahusika katika kuhamasisha wananchi ili washiriki katika mashindano haya.

Mshiriki atatakiwa kujiandikisha kuingia katika shindano kwa kujaza fomu za ushiriki zinazopatikana katika ofisi ya Afisa Mtendaji wa Mtaa/ Kijiji, Kata, ofisi za Halmashauri ya Wilaya/Manispaa/ Jiji nchini na baada ya kujaza fomu husika mshiriki atatakiwa kuirudisha katika Ofisi ya mtaa au kijiji katika eneo lake mahali ambapo mchakato wa kupata washiriki utaanzia.

## AINA YA TUZO NA THAMANI YAKE

| - WASHINDI KITAIFA | TUZO/ZAWADI NYINGINE | |
|---|---|---|
| | FEDHA TASLIMU TSH | ZAWADI NYINGINE |
| Mshindi wa Kwanza | 5,000,000 | Pikipiki na Cheti |
| Mshindi wa Pili | 4,000,000 | Pikipiki na Cheti |
| Mshindi wa Tatu | 3,000,000 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Nne | 1,500,000 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Tano | 1,000,000 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Jumla | 2,000,000 | Ngao |

## UTEUZI WA WASHINDI

### Ngazi ya Mkoa

Uteuzi wa washindi wa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira utaanzia kwenye mikoa husika katika ngazi za kijiji/mtaa, kata, wilaya, mikoa na hatimaye kupata washindi wa kitaifa kwa kila kundi la ushindani.

### Ngazi ya Kitaifa

Katika ngazi hii kutakuwa na **Kamati ya Uteuzi** na **Jopo la Wataalam**. Uteuzi wa mshindi utafanywa baada ya Kamati ya uteuzi kupitia mapendekezo ya Jopo la Wataalamu. Kamati itateua washindi wa kitaifa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kwa hatua mstahiki.

**Kwa maelezo Zaidi tembelea www.vpo.go.tz ama piga simu namba 0784 589610.**

# Serikali yatoa elimu ya madhara ya zebaki

Serikali imewataka wachimbaji wadogo wa dhahabu iwatumie vifaa vya kuwakinga na madhara ya zebaki wakati inaangali namna ya kupata mbadala wa kemikali hiyo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima wakati akizungumza na wachimbaji wadogo kwa nyakati tofauti katika vijiji vya Sambaru wilayani Ikungi na Londoni wilayani Manyoni mkoani Singida.

Sima alisema kuwa Serikali inaendelea na kuwapa elimu wachimbaji hao katika maeneo mbalimbali nchini ili waweze kuepuka madhara ya kiafya yanayotokana na kemikali hiyo.

"Tanzania tuliridhia Mkataba wa Minamata mwaka jana unaotaka kupunguza ama kuondoa kabisa matumizi ya zebaki kwa ninyi wachimbaji ili kuwaepusha madhara ya kiafya na kimazingira katika maeneo yenu," alisema naibu waziri.

Akiwa katika ziara hiyo ambapo alitembela kuona shughuli za uchimbaji na kukagua namna wanavyotunza mazingira, Sima alisema kuwa jukumu la Serikali ni kutoa elimu juu ya madhara ya zebaki ili kulinda afya za wachimbaji wadogo.

"Niwaahidi tu tutashirikiana na Ofisi ya Madini ili muweze kupata vifaa maalumu vya kujikinga wakati wa kuchenjua badala ya mikono, tutawaletea *gloves* mvae mikononi na *musk* wakati tunachoma ili kufunika pua kwani kemikali hii ina madhara kiafya," alisema.

Aidha, Naibu waziri aliwataka wachimbaji hao kuacha kukata miti wakati washughuli za uchimbaji wa dhahabu na badala yake wawe na utamaduni wakutumia njia mbadala kama ambavyo wanavyoelekezwa na mamlaka zinazohusika.

Aliongeza kuwa jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais na Serikali kwa ujumla nikuhakikisha nchi inakabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuleta athari.

Alisema tunapoendelea kuchoma na kukata miti ovyo, kulima kiholela na kuchimba mashimo ovyo kwa ajili ya madini ni mambo yanayosababisha mvua isije kwa wakati pamoja na jua kuwa kali kuliko kawaida.



***Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima akiangalia namna ambavyo uchenjuaji wa dhahabu kwa kutumia zebaki katika mgodi mdogo uliopo kijiji cha Sambaru wilayani Manyoni mkoani Singida ambao unafanyika bila kutumia vifaa maalumu vya kujikinga mikono jambo ambalo linaleta madhara kwa afya na mazingira.***

# Mhe Samia azindua Mtandao wa Viongozi wanawake



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua Mtandao wa Viongozi wanawake Afrika Tawi la Tanzania, Jijini Dodoma ambapo kauli mbiu ya Mtandao huo ni Wanawake na Uongozi Twende Pamoja Wakati ni huu.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Wajumbe wa Mkutano wa Mtandao wa Viongozi Wanawake Afrika kwenye Uzinduzi wa Mtandao wa Viongozi wanawake Afrika Tawi la Tanzania Jijini Dodoma ambapo kauli mbiu ya Mtandao huo ni Wanawake na Uongozi Twende Pamoja Wakati ni huu.*



# Waziri Zungu aipongeza SMZ kwa kuwaletea wananchi maendeleo

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Mussa Azzan Zungu ameipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa usimamizi wao makini wa kuwaletea maendeleo wananchi wa visiwa hivyo.

Zungu alitoa pongezi hizo hivi karibuni alipofanya mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ Balozi Seif Ali Iddi alipomtembelea ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha baada ya kuteuliwa hivi karibuni.

Alibainisha kuwa pamoja na kuwepo kwa changamoto hususana za kimazingira lakini Zanzibar imepiga hatua kimaendeleo sambamba na kuongezeka kwa Pato la Taifa.

Aidha, kutokana na changamoto hizo aliahidi kuteua wataalamu maalum wa masuala ya mazingira kwa lengo la kuangalia athari za mazingira zilizojitokeza katika maeneo tofauti.

Waziri huyo aliahidi kupanga ziara maalum ya kuangalia hali ya mazingira katika maeneo ya Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar inayoratibu na kusimamia mambo ya Muungano na Mazingira kwa upande wa Zanzibar.

Ali Iddi alisema Muungano umenufaisha pande zote mbili za muungano.

Alisema kuwa zipo fursa zinazowanufaisha wananchi wa Zanzibar ndani ya ardhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Bara walioamua kuishi Bara kuendeleza shughuli zao za uwekezaji katika kilimo.

Akizungumza kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Mohamed Aboud Mohamed alimuahidi kumpa ushirikiano katika jitihada za kuhakikisha Muungano unaendelea kuimarika.

# Ofisi ya Makamu wa Rais inavyoendelea kushughulikia changamoto za Muungano




*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Malongo (kushoto) akiendesha kikao kazi cha Makatibu Wakuu kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kujadili masuala ya Muungano.*

Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kushughulikia changamoto za Muungano huku baadhi zikipatiwa ufumbuzi ndani ya miaka minne ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Miongoni mwa changamoto zilizotatuliwa katika kipindi hicho ni kufuta kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika umeme unaotozwa na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kwa Shirika la Umeme Zanzibar (Zeco). Hatua hiyo imeliondolea Zeco mzigo wa kiasi cha shilingi bilioni 22.9.

Mafanikio mengine katika kipindi hicho ni kusimamia utaratibu wa kufuatilia ajira katika wizara na taasisi za Muungano kwa uwiano wa asilimia 79 kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na asilimia 21 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Kuondoa kodi katika unga wa maziwa toka Zanzibar kuja Tanzania bara ni changamoto nyingine iliyokuwa kikwazo lakini sasa hali ni shwari katika eneo hilo.

Changamoto zingine zinaendelea kufanyiwa kazi na ziko kwenye hatua nzuri ya kukamilishwa.

Mbali na kusimamia mazingira nchini, Ofisi ya Makamu wa Rais ndio yenye jukumu la kusimamia masuala ya Muungano.

Katika kufanikisha utendaji, muundo wa wizara umebadilishwa ili kuleta ufanisi katika kusimamia masuala ya Muungano.

Ofisi ya Mratibu wa Muungano huko Zanzibar imepandishwa hadhi na kuwa na Naibu Mkurugenzi wa Muungano. Mabadiliko haya yamesaidia kuongeza ufanisi katika mawasiliano pamoja na kushughulikia changamoto mbali mbali.

**Miongozo na Taratibu**

Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeweka utaratibu wa vikao vya pamoja kati ya SMT na SMZ.

Utaratibu huu unaanzia ngazi ya kamati ya pamoja ya makatibu wakuu SMT na SMZ, kamati ya mawaziri na baadaye kikao cha kamati ya pamoja ambacho mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Kamati ndogo mbili zimeundwa ili kuongeza ufanisi ambazo ni Kamati ya Fedha Uchumi na Biashara, na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Lengo ni kuleta ufanisi katika kushughulikia masuala mahsusi bila kuhusisha vikao vikubwa na kuwa utaratibu huo pia umeweka ratiba ya vikao ili kuhakikisha kwamba vikao vinakaa kama ilivyopangwa.

INAENDELEA UK. 9

# Ofisi ya Makamu wa Rais inavyoendelea kushughulikia changamoto za Muungano

INATOKA UK. 8

**Wizara zisizo za Muungano**

Katika kuhakikisha ushirikiano kati ya SMT na SMZ unakuwa bora zaidi, wizara ambazo sio za muungano zimewekewa utaratibu wa kukutana katika kila angalau robo ya mwaka.

Malengo ya utaratibu huu kwa ni kuangalia changamoto zitakazokuwa zimejitokeza na kuzitafutia ufumbuzi.

Lengo lingine ni kubadilishana uzoefu na taarifa mbalimbali katika sekta zao na hivyo kudumisha ushirikiano hata katika masuala ambayo sio ya Muungano.

Sambamba na hayo Ofisi ya Makamu wa Rais pia imetayarisha Mwongozo wa Ushirikishwaji wa SMZ katika masuala mbalimbali ya kimataifa

**Miradi ya maendeleo**

Katika kipindi cha miaka minne, Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushirikiana vyema katika miradi mbali mbali ya maendeleo.

Baadhi ya miradi hiyo kuwa ni Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (MIVRAF) pamoja na mradi wa kuongeza tija na uzalishaji wa zao la Mpunga (EERP)

Miradi mingine, ni ule wa Udhibiti Uvuvi na Maendeleo shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) pamoja na mradi wa kujengea wananchi uwezo kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (LDCF).

Kwa ujumla Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi hiki cha miaka minne, imeendelea kuhakikisha kwamba Muungano wetu unaendelea kulindwa, kudumishwa, kuendelezwa na kuimarishwa.



***Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi (katikati) akiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Balozi Joseph Sokoine (kushoto) kutembelea eneo la kujenga Ofisi za SMZ jijini Dodoma hatua ambayo itadumisha Muungano.***

# Serikali kuwachukulia hatua wakiukaji sheria

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu amesema Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa wazalishaji na wasambazaji wa mifuko isiyokidhi viwango ili kudhibiti uchafuzi utokanao na mifuko hiyo.

Zungu alitoa kauli hiyo Itigi Wilayani Manyoni mkoani Singida baada ya kushuhudia zoezi la uteketezaji wa zaidi ya tani 11.53 za mifuko mbadala aina ya *non-woven* iliyokamatwa katika mikoa ya Tabora, Singida na Dodoma.

Katika zoezi hilo lililofanyika kwa kutumia kichomeo wananchi kutonunua mifuko isiyokidhidhi viwango vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kufanya hivyo watengenezaji hawatapata soko na hivyo itaisha.

"Mifuko hii ni michafu na inaharibu mazingira, Serikali imeshatoa agizo na sheria imetungwa lakini mifuko hii inarudi hapa wafanyabiashara wana kiburi wanadharau mamlaka na sisi tutachukua hatua stahiki, lakini tutaendelea kutoa elimiu kwa wananchi" alisisitiza Zungu.

Alitoa rai kwa wazalishaji, wasambazaji na wananchi kwa ujumla kuwa ni kosa kisheria kutumia mifuko aina ya *non-woven* isiyokidhi viwango kuchukua hatua kwa mtu yeyote au kiwanda kitakachozalisha mifuko mbadala isiyokidhi viwango vya ubora.

Aliongeza kwa kuhamasisha jamii itumie mifuko yenye viwango kwani watengenezaji wa mifuko hawalipi kodi na inachafua mazingira na pia kutasaidia kuinua viwanda vyetu.

Aidha waziri huyo katika ziara hiyo aliyotumia pia kutembelea masoko na maduka na kutoa elimu kuhusu matumizi ya mifuko mbadala alilielekeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuendelea na ukaguzi wa mifuko isiyokidhi viwango na hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria.

Awali katika taarifa yake Meneja wa Kanda ya Kati wa NEMC Novatus Mushi alisema katika operesheni hiyo, Baraza likishirikiana na wataalamu kutoka TBS, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa husika (REME), Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya husika, Jeshi la Polisi na idara nyingine za serikali walifanya ukaguzi katika maeneo ya masoko, maduka ya bidhaa za vyakula, na stoo za kusambaza bidhaa mbalimbali.

Mushi aliongeza jumla ya tani 3.03 za mifuko iliyopigwa marufuku ilikamatwa.

Aidha, kufuatia operesheni za awali zilizofanywa na NEMC Juni hadi Desemba, 2019 tani 8.5 ilikamatwa hivyo, kufanya jumla ya kiasi cha mifuko iliyokamatwa kufikia tani 11.53.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu akishuhudia zoezi la uteketezaji mifuko isiyokidhi viwango Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida.***

# Utautambuaje mfuko wa non woven wenye viwango?




Ewe Mwananchi tambua kuwa mfuko mbadala unaoruhusiwa ni lazima uwe na viwango vya TBS kama ifuatavyo:

- **Uzito usiopungua GSM 70 (Gram per Square Metre)**
- **Iwe na inaweza kurejelezwa (Recyclable)**
- **Ioneshe uwezo wa kubeba (Carrying Capacity)**
- **Iwe imethibitishwa na TBS**
- **Iwe na jina na anuani ya mtengenezaji**

# Waziri Zungu: Serikali yaendelea kutoa elimu ya mifuko mbadala



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Zungu amesema katika kipindi hiki cha miezi tisa (9) tangu Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga marufuku mifuko ya Plastiki za mwaka 2019 zianze kutekelezwa, Serikali imefanya jitihada za kutoa elimu kwa wadau mbalimbali, kuandaa viwango vya ubora wa mifuko mbadala ya Non-woven, kufanya kaguzi katika maeneo ya uzalishaji, usambaji na uuzaji wa mifuko mbadala.

Akifungua kikao cha wadau katika ukumbi wa LAPF, Kijitonyama chenye lengo la kukuza uelewa wa Sheria na Utekelezaji wa Kanuni ya Katazo la Mifuko ya Plastiki kwa wazalishaji, waingizaji, wasambazaji na wauzaji wa mifuko mbadala Jijjini Dar es Salaam, Zungu ameainisha kuwa mifuko mbadala inayoruhusiwa kisheria kutumika kubebea bidhaa hapa nchini ni lazima ikidhi matakwa ya kisheria.

"Mwongozo umeainisha viwango vya ubora wa mifuko mbadala ya "Non-woven" ni uzito usiopungua 70GSM; iwe inayoweza kurejelezwa (recyclable); iwe na anuani ya mzalishaji au nembo ya biashara (trade mark); ionyeshe uwezo wake wa kubeba (carrying capacity); na iwe imethibitishwa ubora wake na Shirika la Viwango-TBS" Zungu alisisitiza.

Waziri Zungu amesema kuwa hadi sasa tani 54 za mifuko aina ya non-Woven zimekamatwa na kusisitiza kuwa hivi sasa adhabu kali zitatolewa ikiwa ni pamoja na faini, kufunga viwanda na kusisitiza kuwa msako mkali unaanza kwa wazalishaji na wasambazaji wa mifuko isiyokidhi viwango.

"Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Juni, mosi 2019 shehena ya mifuko mbadala isiyokidhi viwango isiyopungua tani 54.035, katoni 12,767 na vipisi 11,191, 919 imekamatwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara wakati wa kaguzi na hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake, zimechukuliwa kwa waliokutwa na makosa. Hatutishani lakini tunatoa tahadhari! Wenye viwanda wanaoendelea kukaidi wakikamatwa watashtakiwa kwa kuhujumu uchumi" Zungu alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Waziri Zungu amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuitisha kikao cha wakurugenzi na Wataalamu wa Mazingira katika Halmashauri zote nchini kuwakumbusha majukumu yao ya kusimamia ipasavyo ka tazo la Mifuko ya Plastiki na kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma.

Naye Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka amesema Serikali imefanikiwa kusimamia katazo la Mifuko ya Plastiki ingawa kuna changamoto ambazo Ofisi yake inazifanyia kazi kwa karibu.

Amesema kuwa changamoto kubwa ni kutojitangaza kwa wafanyabiashara wa mifuko mbadala kwa kutumia vyombo vya habari.

"Inakuwa vita hivi tunapiga sisi wenyewe, tunaowapigania wao wamekaa pembeni, natoa wito kwa jamii kushiriki kikamilifu, tunalinda mazingira kwa vizazi vijavyo, suala hili linahitaji elimu endelevu na sisi tutaendelea kufanya hivyo" amesisitiza Dkt. Gwamaka.

Dkt. Gwamaka amelipongeza Jeshi la polisi Makao Makuu (Kitengo cha Mazingira) kwa mchango mkubwa wanaotoa kwa Baraza ikiwa ni pamoja na kusimamia kikamilifu Katazo la Mifuko ya Plastiki.

Dkt Gwamaka amesema kuwa mpaka sasa Viwanda 72 vya kuzalisha mifuko mbadala vinafanya kazi hapa nchini na kutoa ajira takriban 2761.

# Sima: Wachimbaji tunzeni mazingira



“Eneo hili lipandwe miti ya kutosha ili tutunze mazingira”

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima amewataka wachimbaji wadogo kuhifadhi mazingira katika maeneo yao ya machimbo kwa kupanda miti.

Sima alitoa kauli hiyo akiwa katika ziara yake ya kutembelea wachimbaji wa machimbo ya Sekenke 1 wilayani Iramba mkoani Singida ikiwa ni sehemu ya ziara yake mkoani humo.

Katika ziara hiyo ya kuangalia namna wachimbaji hao wanavyotunza mazingira pamoja na kuwapa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya kemikali ya zebaki alisema ni wajibu kwao kuhakikisha hawakati miti ovyo ili kuepusha changamoto za kimazingira.

“Maisha yetu yanategemea mazingira safi na salama lakini wakati katika eneo hili tumeona miti ni michache, kiafya hii si salama niwaombe mwakilishi wa Mkurugenzi, mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na watu wa madini eneo hili lipandwe miti ya kutosha ili tutunze mazingira,” aliagiza,” aliagiza.

Aidha naibu waziri huyo aliwataka wachimbaji hao kutafuta mbadala wa matumizi ya miti ambayo wanakata kwa ajili ya kuimarisha mashimo wakati wanafanya shughuli za uchimbaji.

Kwa upande mwingine Sima alisema kuwa Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki ulioridhiwa na Tanzania hivi karibuni una kipengele kinachosisitiza uanzishwaji wa vikundi vya wachimbaji.

Alisema hatua ya kuanzisha vikundi itarahisisha ukopeshaji za fedha zikiwemo benki hapa nchini kuliko ambavyo inavyokuwa kwa mmoja mmoja.

“Ndugu zangu ni wakati sahihi ambapo Rais kwa adhamira yake ya kuhakikisha wachimbaji wadogo wanalindwa na tumepokea kodi alizoondoa sasa tupokee namna anavyolinda afya zetu,” alisema.

Kwa upande wake Afisa Mazingira wa Mkoa wa Singida Charles Kidua alisema kuwa takriban hekta laki nne za misitu hupotea kila mwaka kutokana na changamogto ya ukataji.


Kidua alifafanua kwa kusema kuwa ili kuepusha nchi yetu kugeuka jangwa, Serikali imekuwa ikiendelea kuwataka wananchi wapande miti kwa wingi badala ya kuikata.




KWA MAELEZO ZAIDI

**KUPIGA BILA MALIPO**
**0800 110 115, 0800 110 116, 0800 110 117, 0800 110 118, 0800 110 119**

**SMS/WHATSAPP**
**+255 737 796 253, +255 737 796 252, +255 737 796 251 +255 737 796 250, +255 737 796 249**




KWA MAELEZO ZAIDI

**KUPIGA BILA MALIPO**
**0800 110 115, 0800 110 116, 0800 110 117, 0800 110 118, 0800 110 119**

**SMS/WHATSAPP**
**+255 737 796 253, +255 737 796 252, +255 737 796 251 +255 737 796 250, +255 737 796 249**



# Zungu:Mradi wa bomba la mafuta ghafi ni salama kwa mazingira

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Mussa Azzan Zungu hii leo ameshuhudia makabidhiano ya Cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira kwa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la afrika mashariki ikiwa ni hitimisho la ripoti ya Tathmini ya mazingira kwa Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima hadi Bandari ya Tanga.

Amesema mradi huo ni wa bomba lenye urefu wa km1443 kutoka Uganda Wilaya ya Hoima hadi eneo la Chongoleani katika bandari ya Tanga na kwa upande wa Tanzania pekee bomba lina urefu wakilomita1114 ambao ni asilimia zaidi ya 80 zitakazopita katika mikoa Minane (8) na Wilaya 24 nchini "Furaha yangu inatokana na uhalisia kwamba sehemu kubwa ya mradi na vituo viko Tanzania na NEMC wameweza kufanya kazi hii na kumaliza kwa wakati, ambapo kwa upande wa Uganda bado wako kwenye hatua za mwisho. Natumaini hafla hii itawahimiza watendaji na Mamlaka za wenzetu kuweza kukamilisha tathmini hizi za Mazingira kwa wakati Zungu alisisitiza.

Hafla ya kukabidhi Cheti cha Tahtmini ya Mazingira kwa Mradi wa EACOP, ni Ushahidi wa Serikali kuridhia kuwa Mradi huu utahakikisha kwamba masuala ya kiuchumi, kijamii, mazingira, afya na usalama yanashughulikiwa wakati wote wa kipindi cha kupanga, kujenga na uendeshaji wa shughuli za bomba. "Ili kupunguza athari kwa mazingira na jamii njia litakapopita bomba vituo vitawekwa na kuendeshwa kwa umakini ili kupunguza athari yoyote ya kimazingira na kiikolojia", Zungu aliainisha.

Waziri Zungu amesema kuwa kazi ya Serikali kupitia NEMC haiishii kutoa Cheti tu, bali kuendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake kulingana na masharti ya


Ofisi ya Makamu wa Rais
MUUNGANO NA MAZINGIRA
Ewe Mwananchi shiriki katika mashindano ya kuwania
TUZO YA RAIS
YA KUHIFADHI MAZINGIRA
Tuzo ya Rais ni nini?
Hii ni zawadi itakayotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mtu Binafsi, Kaya, kikundi au Taasisi baada ya kubainika anatunza na kuhifadhi mazingira kwenye mtindo wake wa maisha ya kila siku.


Ofisi ya Makamu wa Rais
MUUNGANO NA MAZINGIRA
Ewe Mwananchi shiriki katika mashindano ya kuwania
TUZO YA RAIS
YA KUHIFADHI MAZINGIRA
Madhumuni ya Tuzo
Madhumuni makuu ya Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira ni kuongeza kiwango cha ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi mazingira ili kulinusuru taifa letu na majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira. Kupitia Tuzo hii, wananchi watahamasika kushiriki katika shughuli za kuhifadhi mazingira katika maeneo yao kwa lengo la kuboresha hali ya mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.
Kwa maelezo zaidi piga simu namba 0784 589 610 ama tembelea www.vpo.go.tz
+255 685 333 444
ofisi_ya_makamu_wa rais
Ofisi ya Makamu wa Rais Tanzania
www.vpo.go.tz




| WASHINDI KITAIFA | TUZO NA ZAWADI NYINGINE | |
|---|---|---|
| | FEDHA TASLIMU | ZAWADI NYINGINE |
| Mshindi wa Kwanza | 5,000,000 | Pikipiki na Cheti |
| Mshindi wa Pili | 4 ,000,000 | Pikipiki na Cheti |
| Mshindi wa Tatu | 3,000,000 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Nne | 1,500,000 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Tano | 1,000,000 | Cheti na Ngao |
| Mshindi wa Jumla | 2,000,000 | Ngao |



# Habari katika picha



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akionesha Kitambulisho Kipya cha Mzanzibari Mkaazi baada kukabidhiwa kitambulisho hicho na Afisa wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Jamii Zanzibar Khatib Said Bakari hukoTunguu, Zanzibar.*

*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Azzan Zungu akihamasisha wafanyabaishara ndogondogo kuhusu matumizi ya mifuko iliyokidhi viwango vya ubora alipokuwa akitembelea masoko na maduka Itigi mkoani Singida.*





*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima akiangalia hatua za uchakataji wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo kijiji cha Sambaru wilayani Ikungi mkoani Singida ambapo aliwapa elimu kuhusu namna ya kujikinga wanapotumia kemikali ya zebakia ambayo ina madhara kwa afya na mazingira.*

# Italia yaahidi kuwekeza katika sekta ya mazingira nchini

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Zungu amesema Serikali ya Tanzania iko tayari kuendeleza ushirikiano na Serikali ya Italia katika nyanja za Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Hayo aliyasema Jijini Dar es Salaam mara baada ya kufanya mazungumzo na Balozi wa Italia hapa nchini Mhe. Roberto Mengoni katika Ofisi ndogo ya Makamu wa Rais Mtaa wa Luthuli Jijini Dar es Salaam.

Amesema suala la Mabadiliko ya Tabianchi ni changamoto kubwa duniani kwa hivi sasa na nchi zinazoendelea ndio waathirika wakubwa kutokana na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na nchi zilizoendelea.

Waziri Zungu ametoa wito kwa Serikali ya Italia kuendeleza mashirikiano katika nyanja za udhibiti wa taka na kujenga uwezo katika uzalishaji wa nishati mbadala ili kukabiliana na uharibufu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kwa matumizi ya kuni na Mkaa.

"Serikali ya Rais John Joseph Pombe Magufuli inatekeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua Umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji kwa lengo la kuongeza nishati ya Umeme na kukuza sekta ya viwanda nchini" Zungu alisisitiza.

Alisema kukamilika kwa mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Julius Nyerere utachochea jitihada za Serikali za kupambana na uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji wa miti kwa matumizi ya nishati ya kupikia.

Ameongeza kusema kuwa jitahada za dhati zinatakiwa kuwepo pia katika uzalishaji wa umeme wa nishati ya jua na upepo.

Kwa upande wake Balozi wa Italia nchini Tanzania amesema kuwa nchi yake inalenga kutoa msukumo zaidi katika mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya Tabianchi, kuhimiza kilimo rafiki kwa mazingira, nishati mbadala na nishati jadidifu.

Waziri Zungu amemuhakikishia Balozi Roberto ushirikiano wa dhati katika kupambana na uharibifu wa mazingira nchini ili kuhakikisha Tanzania inabaki salama kwa taifa la sasa na vizazi vijavyo.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu akizungumza na Balozi wa Italia nchini Tanzania Mhe. Roberto Mengoni katika Ofisi ndogo ya Makamu wa Rais Luthuli Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine, nchi hizi mbili zimekubaliana mikakati ya pamoja ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya Tabianchi.***




# Zungu asisitiza matumizi ya mifuko inayokidhi viwango

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Zungu amesema Serikali iko katika tafiti kuhakikisha matumizi ya gesi kama mbadala wa kuni na mkaa yanakuwa ya bei nafuu kwa wananchi wote.

Hayo aliyasema Jijini Dar es Salaam mara baada ya kufanya ziara ya kikazi katika Vyombo vya Habari vya Azam Media na Mwananchi Communications.

Amesema changamoto kubwa hivi sasa ni kukithiri kwa ukataji wa miti kwa matumizi ya kuni na mkaa.

"Tunakuja na programu ya kuweza kulipia gesi kadri unavyotumia (paymetre)" Zungu alisisitiza.

Waziri Zungu amesema kuwa kwa siku mwananchi anatumia sio chini ya shilingi 1500 – 2000 kununulia mkaa, gesi tunayoongelea itagharimu kati ya Shilingi 900-1000 na tafiti zinaendelea ndani ya Serikali kwa kushirikiana na wadau. "Tunataka bei ya gesi ishuke ili wateja wawe wengi ili kunusuru mazingira yetu". Katika hatua nyingine Waziri Zungu amewatahadharisha wananchi kuwa makini na ununuzi wa mifuko mbadala aina ya Non-Woven ambayo haikidhi viwango vilivyoainishwa.

Alisema kuwa mifuko aina ya Non-Woven ni lazima ikidhi viwango vya ubora vilivyoainishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ikiwa ni pamoja na kuwa na uzito usiopungua GSM 70, iwe inaweza kurejelezwa, ionyeshe uwezo wa kubeba na iwe imethibitishwa na TBS. "Nawasihi wananchi wetu kuwa makini na mifuko isiyokidhi viwango vya ubora kwa kuwa ina athari kwa mazingira na kiuchumi. Mifuko inayotengenezwa nchini mingi inakidhi viwango vilivyoweka na hivyo inachangia ulipaji wa kodi na maendeleo ya taifa letu. Mifuko isiyokidhi viwango inatoka nchi jirani na inaua viwanda vya Tanzania" Zungu alisisitiza.


OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA
EWE MWANANCHI..!
Mabadiliko yanaanza na wewe! Mifuko mbadala MPANGO MZIMA.


OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA
MATUMIZI SAHIHI YA MIFUKO MBADALA
EWE MWANANCHI..!
Tumia fursa hii kuwekeza katika mifuko mbadala

# HABARI KATIKA PICHA



**Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Azzan Zungu aliyemtembelea ofisini Vuga, Zanzibar. Wengine ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Mohamed Aboud na Mkurugenzi wa Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.**

***Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima akifafanua mambo mbalimbali katika Kituo cha Radio Standard Singida alipofanya ziara ya kikazi mkoani humo hivi karibuni.***





***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu akikagua eneo la Karakata Mji mpya kujionea uharibifu wa mazingira katika Mto Msimbazi, katika ziara hiyo aliambatana na Mbunge wa Segerea Mhe. Bona Kamoli***


KUMBE ILE MIFUKO MIEUPE LAINIIIIII YA PLASTIKI NAYO IMEPIGWA STOPU EE?
YES, IOGOPE KAMA UKOMA. UKIKUTWA NAYO KALANDINGA LINAKUHUSU


VIBEBEO
TUMENG'ANG'ANIA MIFUKO YA PLASTIKI WAKATI VIBEBEO VIKO KIBAO!!!

Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Makamu wa Rais
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038
Nukushi: +255 266 235 0002
Baruapepe: ps@vpo.go.tz
Tovuti: www.vpo.go.tz
Facebook: ofisi ya makamu wa rais
Instagram: ofisi_ya_makamu_wa_rais
Twitter: @vpo_tanzania
Simu: +255 685 333 444